SAUTI YA NGU

# Toleo Rafiki Kwa Mtoto

## Sheria na Sera za Haki na Ulinzi



UWAJIBIKAJI RAFIKI KWA MTOTO

Sawa Wanawake SAWA Tanzania

ChildFund Korea

## ZIJUE HAKI ZA BINADAMU

Haki za binadamu ni zile stahili ambazo kila mwanadamu anazo au anastahili kuwa nazo kuwa tu yeye ni binadamu. Haki za binadamu ni haki ambazo haziba-gui mtu wa aina yeyote na bila haki hizo hawezi kuwa binadamu kamili.

## MATAMKO YA UMOJA WA TAIFA JUU YA HAKI ZA BINADAMU

***Tamko la kimataifa la hakiza dinadamu la mwaka1948***

Tamko hili limekubaliwa na kupitishwa na baraza kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 10/12/1948 (Hivyo kufanya tarehe 10, desemba kuwa siku ya haki za binadamu duniani). Tamko hili ndilo chimbuko la kulindwa kwa haki za binada-mu duniani kote. Tamko hili linajumuisha kwa pamoja,aina zote za haki za binadamu yaani haki za kiraia, kisiasa, na kitamaduni. Tamko ili linaheshima sana kimataifa na nchi nyingine wamelitambua na kuingiza kwenye katiba zao, Tanzania imefanya hivyo katika ibara ya 90, ya katiba ya mwaka 1977.

## SIFA ZAHAKI ZA BINADAMU

Haki za binadamu zina sifa zifuatazo:-

- Zinalindwa na kuheshu utu na thamani ya kila binadamu
- Hazibagui kwa misingi ya jinsia, rangi, kabila, ukoo, dini, itikadi za kisiasa, uwezo wa mtu kifedha au rika, makundi ya jamii.
- Ni za asili zipobila kutegemea utashi wa mtu au kikundi cha watu.

## UKATILI DHIDI YA WATOTO

***Mtoto:***

Nimtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18, hivyo ukatili wa mtoto maana yake ni ukatili wa iana yoyote ambao ulitokea kabla ya mtoa taarifa hajatimiza umri wa miaka 18.

Unyanyasaji wa kijinsia utotoni,watoto wanapokea vitu au pesa wafanye ngono.

- Ukatili wa kiakili: *Ni kama vile kuitwa majina mabaya, kuonyesha kwamba hutakiwi kwenye jamii fulani.*
- Ukatili wa kimwili: *Ni kama kupigwa fimbo, kofi, kusukumwa, kupigwa ngumi, kuchapwa au kutishiwa na silaha kama bunduki au kisu*.

## MKATABA WA KIMATAIFA WA HAKI ZAKIRAIA NA KISIASA WA 1989

Huu ndio mkataba mkuu unaoshughulikia haki za watoto duniani kote. Mkataba huu ulipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Novemba 1989 na kuanza kufanya kazi tarehe 2 Septemba 1980.Tanzania imeukubali Mkataba huu tarehe 10 Julai 1991.

Haki za mtoto zinazolindwa na mkataba huu

- Haki ya kuishi kwenye mazingira mazuri ikiwemo kupata lishe bora;
- Haki ya kuendelea, kukua ikiwemo haki ya kupata elimu, haki ya kucheza;
- Haki ya kulindwa na wazazi/walezi/jamii au serikali dhidi ya madhara;
- Haki ya kushiriki katika masuala yanayomgusa.

## MKATABA WA KIAFRIKA WA HAKI NA USTAWI WA MTOTO

Mkataba huu ulipitishwa na wakuu wa nchi na serikali za Umoja wa Nchi huru za Afrika (sasa hivi unajulikana kama Umoja wa Afrika) Julai 1990. Mkataba huu umeanza kufanya kazi tarehe 29 Novemba 1999. Hadi Agosti 2004, nchi 35 kati ya nchi 53 za Afrika zimeuridhia, Tanzania imesaini mkataba huu tarehe 3/10/1998 nakuuridhia tarehe 16/03/2003.

## UKATILI WA KIJINSIA

Nitendo analotendewa mtu mwingine bila idhini yake ambalo linaunganisha makosa ya kujamiana bila ridhaa (kubakwa) kumgusa kijinsia pasipo ridhaa au kutomasa (kumgusa sehemu asizotaka) na unyanyasaji bila kugusana (Mfano: vitisho vya kutumia nguvu kijinsia, ujitwazaji kingono, kubugudhi kwa maneno ya kijinsia).

Ripoti ya ukatili dhidi ya watoto Tanzania 2011 **(Serikali na UNICEF)**

Jedwali: Wakosaji waukatili wangono kamaulivyoripotiwana mwenye umri kati ya 13na 24. **(RUDWT 2009)**

| Mshambuliaji | Wasichana | Wavulana |
|---|---|---|
| Jirani | 32.2% | 16.6% |
| Mtu siyejulikana | 32.0% | 25.7% |
| Mwandani | 24.7% | 47.9% |
| Mwenye mamlaka juu ya muhanga | 14.7% | 2.8% |
| Rafiki/Mwanafunzi | 10.3% | 8.6% |
| Ndugu wa ukoo | 7.1% | 14.7% |

## HAKI ZA BINADAMU KWA MUJIBU WA KATIBA YA JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Usawa wa binadamu:**
Kifungu cha 12 (1) Binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa kifungu 12 (2) kila mtu anastahili kuheshima ya kutambuliwa utu wake kifungu 13 (1) “usawa mbele ya sheria”. Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.

**SHERIA YA HAKI ZA WATOTO No. 21 (2009)**
Sheria hii ya mtoto inazungumzia:-

- ·Sheria za mtoto · Haki za mtoto
- ·Kulinda, kukuza na kuhifadhi ustawi wa mtoto
- ·Masharti ya unasibishaji wa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa ·
- Maswala ya kulea, kuasili na ungalizi
- ·Pia, inatoa maelezo na masharti yanayohusu mtoto anapokuwa katika mgogoro wa sharia.

**HAKI ZA WATOTO**
***Haki ya kutotengwa***
Mtoto atakuwa na haki ya kuishi huru bila kuwepo namna yoyote ya kutengwa yaani kuonekana kuwa hastaili kujumuika na wenzake katika kundi.
Mtu yeyote haruhusiwi kumtenga mtoto kwa sababu;-
Jinsi, rangi, umri au dini mtu hatakiwi kumtenga mtoto kwa sababu anaongea lugha tofauti: Mtoto hatakiwi kutengwa kwa sababu ametoa maoni tofautiya kisiasa.

- Mtoto hatakiwi kutengwa kwa sababu ni mlemavu au kwa hali yake ya kifya.
- Mtoto hatakiwi kutengwa kwa sababu ya hali yake ya kijamii au kiuchumi.

**Haki ya jina na utaifa**
Mtoto ana haki ya kujua jina lake, utaifa na wazazi wake waliomzaa, na ukoo wa familia yake.

## HAKI ZA WATOTO

**Haki ya kuishi na wazazi au walezi**

Mtoto ana haki ya kuishi na wazazi au walezi wake. Mtu yeyote haruhusiwi kumnyima mtoto haki ya kuishi na wazazi, walezi au familia yake. Pia ni haki ya mtotokukuwa katika malezi na mazingira ya amani.

**Wajibu wa kutunza mtoto**

Niwajibu wa Mzazi/Mlezi au mtu yeyote mwenye kumlea mtoto kutoa mafunzo kwa mtoto.

**Wajibu huu hasa humpatia mtoto haki ya:-*

- Chakula
- Mavazi
- Malezi
- ¨Dawa na chanjo
- Elimu na mafunzo
- Uhuru
- Haki ya kucheza na kupumzika



## HAKI ZA WATOTO

***Haki ya kupata huduma***

Mtu yeyote haruhusiwi kumnyima mtoto haki ya elimu, chanjo, chakula, mavazi, malazi huduma ya afya na dawa au kitu chochote kinachohitajika kwa ajili ya maendeleo ya mtoto.

**Haki ya kushiriki michezo na shughuli za kiutamaduni**

Mtu yeyote harusiwi kumnyima mtoto haki kushiriki katika michezo au shughuli njema za kiutamaduni na kisanii au za starehe, haki hiyo inaweza isitolewe kama itakuwa na madhara kwa watoto.

## WAJIBU NA JUKUMU LA MZAZI

1. Mtoto atakuwa na haki ya kuishi kwa hadhi, heshima, uhuru, afya, kupumzika na kupatiwa elimu na malazi kutoka kwa wazazi.
2. Kila mzazi anawajibu na majukumu kwa mtoto. Wajibu na majukumu hayo yamewekwa kwa mujibu wa sheria.

**Yanahusisha wajibu wa:**

Kulinda mtoto dhidi ya kutelekezwa, kufanyiwa vurugu, kunyanyaswa, na kuwa katika mazingiramabaya kimwili na maadaili.

1. Kutoa maelezo, uangalizi na msaada na hifadhi kwa ajili ya mtoto.
2. Kuhakikisha kuwa mzazi
3. anapokuwa mbali mtoto, mtoto anapata ungalizi kutoka kwa mtu mwenye uwezo wa kumtimizia majukumu hayo.

## KULINDA MTOTO ASITESWE NA KUDHALILISHWA

- Mtu yeyote haruhusiwi kumfanya mtoto apate mateso au adhabu ya kikatili, ya kinyama auafanyiwe matendo yenye kumshushia hadhi.
- Hii pia ni pamoja na desturi zozote za mila zenye kudhalilisha utu wa mtoto au zinazosababisha athari za maumivu ya mwili au akili ya mtoto.







## WAJIBU WA JUMLA WA MTOTO

Mtoto ana haki lakini pia anawajibu je, wajibuhuo ni upi?
a) Kufanya kazi kwa ajili ya mshikamano wa familia.
b) Kuwaheshimu wazazi, walezi, wakubwa wake na watu wazima na kuwa saidia pale inapohitajika.
c)Kuhudumia jamii yake na taifa lake kwa uwezo wake wote, kimwili na kia-kili kadri ya umri na uwezo wake.
d)Kutunza na kuimarisha mshikamano wakijamii na taifa.
e) Kutunza na kuimarisha mambo mema katika utamaduni wa kijamii na taifa kwa ujumla katika uhusiano wa jamii au taifa.

## HAKI ZA MTOTO,WAZAZI WANAPOTENGANA

Kwa kuzingatia sheria ya ndoa, wazaziwanapotengana au wanapotalikiana mtoto atakuwa na haki ya:-
a)Kupata matunzo na elimu yenye hadhi kama ilivyokuwa kabla wazazi ha-wajatengana au kutalikiana.
b)Kuishi na mzazi ambaye kwa maoni ya mahakama ana uwezo wa kumlea na kumpatia matunzo kwa kiwango kinachostahili kwa ustawi wa mtoto.
c)Kumtembelea na kukaa na mzazi mwingine kila anapohitaji, isipokuwa kama mpango huo utaathiri ratiba ya shule au mafunzo kwa mtoto.

## KUASILI MTOTO

Maombi ya kuasili mtoto yanatoka wapi?
i. Maombi ya kuasili mtoto yanaweza kufanywa mahakama kuu.
ii.Maombi ya “Kuasili kwa wazi” yatafanywa katika mahakama ya hakimu mkazi au mahakama ya Wilaya.
iii.Maana ya kuasili kwawazi ni kusili mtoto kunakofanywa na ndugu.

## MAOMBI YA KUASILI

Maombi ya kuasili mtoto yanaweza kufanywakwa pamojana:-
a)Mume na mke
b)Mama au baba wa mtoto peke yake au pamoja na mwenza wake.

## KURITHI MALI

Je, mtoto aliyeasiliwa atarithi mali ipi?
i. Pale mzazi wa kuasili anapofariki bila kuacha wosia, mali zakezitakuwa mali za mtoto wa kuasili kama vile mtoto amezaliwa na wazazi wa kuasili.
ii. Kwa ajili ya kuondoa utata mtoto wa kuasili hatastahili kurithi mali kama wazazi wa kibailojia wakifa bila kuacha wosia.

## AJIRA KWA MTOTO

i. Mtoto atakuwa na haki ya kufanya kazi nyepesi
ii. Pamoja na kwamba mtoto ana haki ya kufanya kazi nyepesi, umri wa chini utakuwa miaka 14.

## KAZI NYEPESI NI ZIPI?

Kazi nyepesi itahusisha kazi ambayo haiwezi kuwa na madhara kwa afya ya mtoto au maendeleo yake, kazi hiyo haitamzuia au kuathiri maendeleo ya shule katika shughuli za kujiendeleza kiufundi, kozi ya mafunzo au uwezo wa mtoto kunufaika na kazi ya shule.

## AJIRA ZA HATARI

Sio halali kisheria kumuajiri au kumuhusisha mtoto kwenye kazi ya hatari.

## AJIRA ZA HATARI NI ZIPI?

Kazi ya hatari ni kazi yeyote inayoweza kuleta hatari kwa afya, usalama na maadili ya mtoto. Kazi za hatari ni kama:-
a. Kuuza baa na madawa ya kulevya
b. Kufanya kazi kwenye migodi na viwandani

## MTOTO MWENYE MGOGORO NA SHERIA

i. Kutakuwa na mahakama ya watoto itakayokuwa na madhumuni ya kusikiliza na kuamua maswala yanayohusu watoto.
ii.Mahakama ya watoto itaongozwa na hakimu mkazi.

## MAHAKAMA YA WATOTO INAFANYA NINI?

i. Mahakama ya watototoitakuwa na uwezo wa kusikiliza na kuamua.
A. Mashtaka ya jinai dhidi ya watoto
B. Maombi yanayohusu matunzo, kujikimu na kuwalinda watoto.

Je, mahakama zinalindaje mtoto akishtakiwa?
Mahakama ya watoto itakaa mara kwa mara kufuatana na ulazima.
A. Mashauri yatakuwa ya kawaida
B.Mashauri yataendeshwa kwa faragha.
C.Ofisa ustawi wa jamii atakuwepo na kuendesha mashauri
D. Ni haki ya mzazi, mlezi au ndugu kuwepo







**S.L.P 6031, Morogoro, Tanzania**
**Simu: +255 713 514989 au +255 655 000421**
**Barua pepe: sawa98@gmail.com**
**Tovuti: sawawanawake.or.tz**
**Mitandao ya Kijamii: @sawawanawaketz**